

BONDE

HARAKATI ZA NGETI




KIMETENGENEZWA NA
TAI STUDIO

KATIKA KIJIKI CHA IMANI, KULIKUWEPONA BINTI MPOLE, MTARATIBU, MWEREVU DARASANI ILA MWENYE HUZUNI NYINGI, AITWAYE MAGDE.



HAYA MAISHA
MPAKA LINI? MI SIWEZI
KUPIGWA KILA SIKU, KISA
KULAZIMISHWA KUOLEWA.
SIWEZI!!




MAGDE ALIKUWA ANAPITIA HALI NGUMU KIHISIA NA KIMWILI CHINI YA BABA YAKE ALIYEKUWA MKALI SANA - AKIMFANYIA UKATILI, KWA KUMPIGA VIBAYA KWA MAKOSA MADOGO.



KHAAAAA!!


LWIII...
MEUUU WANGUUU.



LIZEMBE
LIMEKUJAAA!
MPUUIZI WEWE.



BABA MAGDE ALINUIA KUMWOZESHA MAGDE KWA MWANAUME MKUBWA BILA RIDHAA YAKE.



BAADA TU YA KUFIKISHWA NYUMBANI, UKATILI HAKUISHA, MAGDE ALIENDELEA KUFANYIWA UKATILI NA MWANAUME ALIEMUOA.



NIMEKWAMBIA NATAKA KULA KABLA YA SAA SABA, MPAKA SASA HAUJAPIKA! UNADHARAU EH?




NILIKUWA NACHOTA MAJI TOKA ASUBUHI, UWII!






TCH!!...
NA UKIENDA KWA BABA YAKO, NITAKUJA KUDAI MAHARI YANGU.

KWA KUKOSA SULUHU KUEPKANA NA UKATILI HUU, MAGDE
ALICHUKUWA MAAMUZI YA KUKIMBILIA NYUMBANI KWA BABA YAKE.



BONDE LILIKUWA NI KIMBILIO LA MADGE, ALIYESIMAMA KATIKA KINGO ZAKE, AKIWA NA HAJA MOJA TU, KUCHUKUA UHAI WAKE MWENYEWWE, KUONDOKANA NA UKATILI ANAOPITIA.





NGETI LICHA YA KUWA MTETEZI WA HAKI ZA MABINTI, ALIKUWA NA HAIBA YA USULUHISHI NA "UDIPLOMASIA", ALITAMANI KUSULUHISHA MGOORO BAINA YA MAGDE NA BABA YAKE.



SAUTI YA BABA MAGDE, NZITO
NA YA UKALI INASIKIKA KWA MBALI.

WEWE
LIMEKUWA MPULUZI
KIASI HIKI

!?

NGETI
LIMEMWAMBIA BABA
NIKO HUKU!

IMEBIDI NIMWAMBIE,
ILI TUYAWEKE SAWA,
HAMUWEZI KUISHI
HIVI KAMA FAMILIA.



MAGDE ANAONEKANA KALIMIZWA.

HUFF

HALAFU WEWE
UMEMFUNDISHA MAGDE
UTUKUTU.

HASIKILIZI
WAKUBWA NA AMEKUWA
MJEURI KAMA WEWE,
NJOO HAPA!

NGETI NA BABA MAGDE WANATOA MACHO KWA KUOGOPA MAGDE ANADONDOKEA BONDENI.

HEEEEE!



AAAAAH!


MAGDEEE!



NIPE MKONO!



NGETI ANAJITAHIDI KUDAKA MKONO WA MAGDE KUMUOKOA ASIANGUKE.



MAGDE ANABAHATIKA KUDONDOKEA UKINGO MDOGO WA BONDE, UNAOMLUOKOA KUPOROMOKA MPAKA CHINI.






MMM...
HAJA DONDOKEA MBALI,
NAWEZA KUMUOKOA.

SASA,
TUNAFANYAJE KUOKOA
MAISHA YA MWANANGU?

HII KAMBA
NAONA ITAFAA...



HII KAMBA
NAONA ITAFAA...



BABA MADGE
JITAYARISHE KUVUTA KAMBA
KWA NGUVU ZAKO ZOTE,
ILI TUMWOKOE
MAGDE.

NGETI ANAMUELEKEZA BABA MAGDE MAHALI PA KUFUNGA KAMBA ILI IMSHUSHE KWENYE BONDE.




KILA MMOJA ANACHANGAMKA KUFANYA WAJIBU WAKE WA KUFUNGA KAMBA ILI WAVEZE KUMUWAHI MADGE KWENYE BONDE.

NGETI AKIWA AMEJIFUNGA KAMBA KIUNONI.



MAGDE
TULIA HIVYO HIVYO,
TUNAKUJA KUKUOKOA..



NIKIKWAMBIA VUTA,
UTAVUTA KAMBA KWA NGUVU
ZAKO ZOTE!
SAWA BABA MAGDE?



NGETI ANASHUKA KWA KAMBA KUMFWATA MAGDE
ALIELALA KWENYE LIKINGO MDOGO WA BONDE.



BABA MAGDE ANAVUTA KWA NGLUVU ZAKE ZOTE.



FRWAAHHH




NGETI NA MAGDE WAKIVUTWA KWA KAMBA NA BABA MAGDE.

BAADA YA KUFIKA JUU MAGDE ANAJISOGEZA TARATIBU KUPANDA AKIVUTWA MKONO NA NGETI.




MAGDE MWANANGU...



NGETI ANAVUTA PUMZI HUKU AKIWAANGALIA MAGDE NA BABA YAKE.

POLE SANA MWANANGU.





AHSANTE NGETI...
AHSANTE. NAOMBA KATAFUTE
MSAADA, TUMUWAHISHE MAGDE
HOSPITALI.


NGETI ANAKIMBIA MPIO KWENDA MTAANI KUOMBA MSAADA WA WATU
WAJE KUMPA HUDUMA YA KWANZA MADGE NA KUMUWAISHA HOSPITALI.



BABA MAGDE ANAMKUMBATIA KWA HISIA
KALI MAGDE.



NISAMEHE MAGDE.
NISAMEHE SANA. SIKUJUA
NAKUUMIZA KIASI HIKI.
HAUTOUMIA TENA NA KUTESEKA
KWA MKONO WANGU.
POLE MAGDE!



KITABU HIKI
KIMETENGENEZWA NA **TAI STUDIO** KWA
KUSHIRIKIANA NA SHIRIKA LA **UNFPA** KWA AJILI
YA VIJANA WA RIKA BALEHE KUJIFUNZA NA
KUELEWA KUHUSU ATHARI ZA UKATILI WA KIJINSIA
NA NDOA ZA UTOTONI. BAADA YA KUSOMA KITABU HIKI,
VIJANA WA RIKA BALEHE WATAJIFUNZA ATHARI HIZI NA
KUPATA MWAMKO WA KUJILINDA NA KUCHUKUWA
TAHADHARI.

WASHIRIKI



Tai
Storytelling for Social Change



UNITED NATIONS
TANZANIA



PRINTED BY TCRS